

MAELEZO YA MSINGI KUHUSU UPANDAJI WA MAZAO KWA NAFASI INAYOSTAHILI

Upandaji wa mazao kwa nafasi huyawezesha kukua kwa afya nzuri na hatimaye kutoa mazao ya kutosha. Miti ama mbogamboga ikisongamana sana haiwezi kukua vizuri na hutoa mazao kidogo, pia magonjwa huishambulia kwa wingi na kiurahisi. Hunyang'anyana maji na virutubisho na pia mwanga wa jua. Vyote hivi ni muhimu kwenye uzalishaji wa aina yeyote ya mazao.

Vilevile miti ama mbogamboga iliyopandwa kwa kuachana sana husababisha mkulima apate mazao kidogo na ardhi kutotumika ipasavyo.

Mazao yaliyopandwa kwa nafasi nzuri hutumia maji na virutubisho vilivyopo ardhini na kuzaa vizuri na hayashambuliwi na magojwa kiurahisi.

Hata hivyo nafasi za upandaji wa zao moja na jingine hutofautiana kulingana na uwezo wa zao wa kutoa majani na mizizi na mahitaji ya virutubisho. Mfano mchicha huchukua nafasi kidogo kutoka mmea na mmea ukilinganisha na kabeji. Pia miti kama korosho huhitaji nafasi kubwa kutoka mti na mti kuliko mahindi.

NAFASI ZINAZOSTAHILI KWA UPANDAJI WA MAZAO MBALIMBALI.

Nafasi kwa sm	Choroko	Muhogo	Mbaazi	Karanga	Mahindi	Korosho	Kunde
Mmea x Mmea	8-12 sm	M 1	Sm 65	Sm 20	Sm 35	M 6 -12	Sm 8-12
Mstari x Mstari	45 sm	M 1	M 1.2	Sm 30 -40	Sm 70	M 12	Sm 30 - 40
Mstari x Mmea	45 x 8 sm au 40 x12 sm	M 1 x 1 au 100 x100sm	120 x 65sm	40 x 20 sm au 30 x 20sm	70 x 35sm	M 12 x12 au M 12 x6	Sm 40 x 8 au Sm 30 x 12

KUHAMISHA MICHE

Miche ikiwa tayari yafuatayo yazingatiwe.

- Ihamishiwe kwenye shamba/bustani iliyoandaliwa mapema.
- Miche iliyo bora tuu ndio ihamishwe
- Epuka miche yenye waduu na au iliyoshambuliwa na magonjwa
- Mwagilia maji ya kutosha masaa 24 kabla ya kuhamisha
- Zingatia upandaji kwa nafasi.
- Weka matandazio ili kuhifadhi unyevu, joto na kuzuiya magugu.
- Hamisha miche wakati wa jioni
- Mwagilia maji ya kutosha
- Wekea kivuli miche iliyohamishwa kuizuiya na jua ama mvua ya moja kwa moja
- Epuka kuitikisa sana miche wakati wa kuihamisha.
- Usikunje mizizi wakati wa kupanda miche